# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Chuo Cha Ualimu Kabanga,
S. L. P. 265,
**KASULU.**

SIMU: **0765873099**
E-Mail: kabangatc@moe.go.tz

Kumb. Na. KBCCU/GFO/186/XI/ 256

Bw/Bi__________________________________________________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU MAALUMU KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

1. **UTANGULIZI:**
Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu kwa mwaka wa masomo 2026/2027. **Hongera sana!.**
Mafunzo haya yatachukua muda wa miaka miwili, kuanzia **2026/2027** hadi **2027/2028** kwa wale ambao watakaa chuoni moja kwa moja na Miaka **(03 hadi 04)** kuanzia **2026/2027 hadi 2028/2029** kwa wale watakaosoma Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu kwa njia ya Masafa. Chuo kitafunguliwa tarehe **17/08/2026** Unatakiwa kuripoti Chuoni kuanzia tarehe **17/08/2026** mpaka tarehe **26/08/2026.** Nakutahadharisha kuwa ukiripoti Chuoni baada ya Tarehe **26/08/2026 hutapokelewa.** Nafasi yako itajazwa na waombaji wengine.

2. **Mahali Chuo kilipo**:
Chuo Cha Ualimu Kabanga kipo Mkoa wa Kigoma Wilaya ya Kasulu. Kwa wanachuo wanaotokea Mikoani kupitia njia ya Kahama/Kagera, Kakonko na Kibondo watapaswa kushuka eneo la majengo mapya ya Chuo cha Ualimu Kabanga yaliyopo eneo la Mubondo, kwani Chuo kipo njiani kilometa 12 kabla ya kufika Kasulu mjini.
Kwa wanaotokea Mikoani kupitia barabara ya Tabora-Uvinza na Kigoma mjini watashukia stendi ya mabasi Kasulu mjini ambapo kuna usafiri wa mabasi madogo (hiace), bajaji au pikipiki kutoka Kasulu mjini kuja Chuo cha Ualimu Kabanga kupitia barabara inayoelekea Kibondo.

**Tanbihi:**
- **Angalizo kwa wale wanaotokea kahama, Usipande magari yanayokwenda Ngara, kuna Kabanga nyingine Wilaya ya Ngara-Kagera**
- **Pia utakapofika Kasulu mjini hakikisha unawapa maelekeo ya kupelekwa Chuo cha Ualimu Kabanga kilichopo eneo la Mubondo na sio Kabanga ya zamani iliyopo kijiji cha Kabanga.**

## 3. MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

i. Cheti halisi cha kuzaliwa na kivuli chake (Photocopy)

ii. Cheti halisi cha kumaliza kidato cha nne (Secondary School Leaving Certificate) chenye picha iliyogongwa Muhuri wa shule na kivuli chake (Photocopy)

iii. Cheti halisi cha kitaaluma cha kidato cha nne (Academic certificate) na kivuli chake (Photocopy)

iv. Cheti halisi cha **kumaliza** kidato cha sita au Ualimu daraja la III A (**Leaving Certificate**) chenye picha iliyogongwa Muhuri wa shule/Chuo na kivuli chake (Photocopy)

v. Cheti halisi cha **kitaaluma** cha kidato cha sita au Ualimu daraja la III A (**Academic certificate)** na kivuli chake (Photocopy) au Original Result Slip kwa wale waliohitimu Kidato cha sita mwaka 2026. **Usije na matokeo yaliyotolewa kivuli toka kwenye kitabu cha matokeo ya mtihani**.

vi. Kitambulisho cha kupigia kura/NIDA na Bima ya afya kwa wale wenye nayo na wale ambao hawana bima ya afya unalazimika kuja na fedha kiasi cha Shilingi **50,400/=** kila mwanachuo kwa kila mwaka.

vii. Uje na barua hii ya maelekezo ya kujiunga (Joining Instructions) wakati wa kuripoti Chuoni ikiwa imejazwa sehemu ya Daktari.

viii. Kwa mwalimu kazini anapaswa kuja na barua ya ruhusa kutoka kwa mwajili wake watakaosoma miaka miwili.

## 4. ADA NA MICHANGO:

Unatakiwa kulipa ada na michango ifuatayo, isipokuwa pale ambapo Wizara itatoa maelezo ya Ufadhili wa Wanachuo wa Kozi hii kwa mwaka husika:-

### ADA:

Ada ya mafunzo kwa mwaka ni Tshs. **450,000/=**. Hivyo kwa muhula wa kwanza unatakiwa kulipa Shs. **225,000/=)** ili usajiliwe na nusu nyingine muhula wa pili. Ada italipwa kwa utaratibu wa kupewa namba maalumu ya utambulisho (**Control Number)** na Mhasibu wa Chuo baada ya kufika Chuoni.

**(a) Michango Mingine kwa Wanachuo Wanaosoma Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu kwa miaka Miwili:**

| S/N | Aina ya mchango | Kiasi | Maelezo |
|---|---|---|---|
| **1** | Serikali ya wanachuo | 5,000/= | Kwa mwaka |
| **2** | Huduma ya kwanza | 10,000/= | Kwa mwaka |
| **3** | Usafi wa mazingira | 20,000/= | Kwa mwaka |
| **4** | Kukodi godoro | 10,000/= | Kwa mwaka |
| **5** | Usajili na kitambulisho | 20,000/= | Kwa mwaka wa kwanza tu |
| **6** | Michezo | 30,000/= | Kwa mwaka |
| **7** | Ulinzi | 30,000/= | Kwa mwaka |
| **8** | Ukarabati | 25,000/= | Kwa mwaka |
| **JUMLA** | | **150,000/=** | |

**(b) <u>Michango Mingine kwa Wanachuo Wanaosoma Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu kwa njia ya Masafa Miaka (03 hadi 04):</u>**

| S/N | Aina ya mchango | Kiasi | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1 | Serikali ya wanachuo | 5,000/= | Kwa mwaka |
| 2 | Huduma ya kwanza | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 3 | Usafi wa mazingira | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 4 | Ufuatiliaji na uendeshaji wa Mafunzo | 40,000/= | Kwa mwaka |
| 5 | Usajili na kitambulisho | 20,000/= | Kwa mwaka wa kwanza tu |
| 6 | Michezo | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 7 | Ukarabati | 25,000/= | Kwa mwaka |
| **JUMLA** | | **150,000/=** | |

**Michango hii ilipwe kupitia Akaunti maalumu ya Chuo. Kupitia Benki yoyote ya NMB**
**<u>Jina la Akaunti</u>: KABANGA TEACHERS' COLLEGE - MAENDELEO ACCOUNT. A/N. 51403500086.**
**Michango yote ilipwe muhula wa kwanza (kabla ya usajili)**

**<u>ANGALIZO:</u>**

**1. Hakikisha unamweleza mpokea fedha wa benki (Bank Teller) kuwa fedha uliyoweka ni ya Michango na aandike Jina la Mwanachuo anayelipiwa kwenye "Bank-pay-in-Slip" sehemu ya Saini ya mwenye Akiba.**

**2. Ili kuepuka Usumbufu, kila fedha ilipwe kupitia Akaunti husika. Yaani ada kwa "Control number" na michango kwenye maaendeo akaunti. Bank-pay in-Slip izalishwe kivuli (Photocopy) na nakala halisi ziwasilishwe Ofisi ya Msajili wa wanachuo mara ufikapo Chuoni.**

## 5. <u>VIFAA MUHIMU:</u>

**Uje na vifaa vifuatavyo**:-

i. Shuka 2 za rangi ya Pinki kwa wasichana na light bluu kwa wavulana (zisiwe na maua)
ii. Blanketi 1, Mto na Foronya inayoendana na rangi ya shuka
iii. Chandarua ni lazima kuna mbu wengi wakati wote
iv. Ndoo na beseni kwa ajili ya kuhifadhia maji na kufanyia usafi
v. Vyombo vya kulia chakula sahani, bakuli, kikombe na kijiko.
vi. Vifaa vya michezo Bukta kwa wavulana na Sketi fupi kwa wasichana, track-suit rangi ya light blue, jozi ya raba na soksi ndefu rangi ya bluu (kwa wote).

## 6. <u>SARE YA CHUO</u>: (Unapaswa kushona mwenyewe)

**<u>WAVULANA:</u>**

i. Mashati mawili ya Blue bahari mikono mirefu.
ii. Suruali mbili rangi nyeusi na koti lake (Angalia kiambatata **Na. 01**).
iii. Tai ndefu rangi nyeusi ifike unapovalia mkanda wa suruali.
iv. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba
v. Mkanda mweusi wa kuvalia suruali.
vi. Soksi nyeusi ndefu jozi 3.
vii. T-shirt yenye nembo ya Chuo inapatikana Chuoni kwa Tsh**. 15,000/=**

**WASICHANA:**


i. Mashati Mawili ya Blue bahari mikono mirefu.
ii. Sketi mbili za rangi nyeusi za rinda box moja na koti lake **(Kitambaa Kizito)** na ziwe ndefu na zisizo bana. (Angalia kiambata **Na. 01**),
iii. Tai fupi ya rangi nyeusi itakayoishia chini ya kitovu.
iv. Viatu vyeusi vya ngozi kisigino kifupi vya kufunga kamba
v. Soksi nyeupe ndefu.
vi. Wanachuo Waislamu wataruhusiwa kuvaa juba inayofanana na rangi ya shati.
vii. T-shirt yenye nembo ya Chuo inapatikana Chuoni kwa Tsh. **15,000/=**

**Tanbihi**

- Endapo hautakuwa na uhakika wa sare sahihi ya chuo, unashauriwa kushughulikia sare baada ya kufika chuoni.
- Uje na nguo chache za heshima.
- Mahitaji na vifaa karibu vyote vinapatikana katika mazingira ya chuo kwa bei sawa na maeneo mengine.

**PICHA NA MCHORO WA SARE ZA CHUO (KIAMBATA Na. 01)**





7. **TAALUMA:**

**Uje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya matumizi binfsi**

(i) Daftari (counter books) za kutosha, zipatazo 14.
(ii) Kalamu za wino za kutosha muhula mzima.
(iii) Rula, Mkebe wa Hisabati (Mathematical set) moja.
(iv) File Cover 10 kwa ajili ya mkoba wa kazi wa kutunzia kumbukumbu na nyaraka za kitaaluma kwa kila somo.
(v) Rimu mbili **A4** aina ya **Double A**

8. **MITIHANI:**

Chuo hutoa mitihani, unatakiwa ufaulu mitihani yote itakayotolewa na Chuo.

9. **AFYA:**

Chuo hakitagharamia matibabu ya mwanachuo (zaidi ya huduma ya kwanza) wakati wa mafunzo yake. Hivyo unashauriwa uje na kadi ya Bima ya afya. Huduma za matibabu zinapatikana Hospitali ya wilaya ya Kasulu.

Kabla ya kuripoti Chuoni hakikisha unapimwa afya yako na Mganga Mkuu **wa Hospitali ya Serikali kuthibitisha kama afya yako inakuruhusu** kuchukua Mafunzo ya Ualimu.Wajawazito hawatapokelewa. Aidha Chuo hakina huduma ya chakula maalum (Special-Diet) kwa wanachuo wenye matatizo ya chakula.

10. **KANUNI ZA CHUO:**

- Mwalimu ni mfano mzuri wa kuigwa na jamii, Chuo kinakutarajia kuwa na sifa za Mwalimu utakapoingia Chuoni na kumaliza mafunzo yako.
- Utapewa mafunzo kabilishi (Orientation) juu ya sheria na taratibu zote za chuo mara ufikapo Chuoni. Aidha utapewa fomu ya kujaza kukubaliana na sheria na taratibu hizo.


**Tanbihi:** Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na Uongozi wa Chuo kupitia namba zifuatazo;-

1. **Ponsian M. Revocatus -Kaimu Mkuu wa Chuo -0765873099**
2. **Chiku Ndama -Mkuu wa Idara ya Udahiri, Mitihani na Vyeti -0766800005**
3. **Philemon Rushaga -Mkuu wa Sehemu ya Utoaji Vyeti -0683021845**
4. **Philbert Katabazi -Mratibu wa Masuala ya Kitaaluma -0753589187**

11. **MWISHO**

Nakutakia maandalizi mema, zingatia sana maelekezo yaliyotolewa.

Ninakutakia kila la kheri na **KARIBU SANA CHUONI.**




**Nakala:** Mkurugenzi,
Elimu ya Ualimu,
Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia,
S. L. P. 10,
**DODOMA.**

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**

Website: ___
Email:kabangatc@moe.go.tz
Phone No.: +255765873099
In reply please refer:

Principal,
Kabanga Teachers College,
P.O.Box 265,
**KASULU-KIGOMA**

**Ref.No. KBCCU/GFO/186/XI/ 257**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A:**

To the Medical Officer;

……………………………………………..

Please examine *Mr/Mrs/Miss ………………………………………. (Name in Full) as to his/her physical and mental fitness for enrolment as a student teacher. The examination should include but not limited to the following categories:

1. (a) Eye sight
   (b) Hearing
   (c) Speech
   (d) Venereal Diseases
   (e) Leprosy
   (f) Limbs
   (g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other medical condition.
4. Blood Group
5. Pregnancy (if applicable)

Date: …………………………. Signature……………………

**PARTB: MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by Government Medical Officer)

1. (a) Eye sight ……………………………………………………………
   (b) Hearing ………………………………………………………………....
   (c) Speech ……………………………………………………………...…..
   (d) Venereal Diseases …………………………………………………………
   (e) Leprosy ……………………………………………………………………….
   (f) Limbs ……………………………………………………………………………….
   (g) Epilepsy ……………………………………………………………………………….
2. Neuroses………………………………………………………………………………
3. Other medical condition…………………………………………………………….
4. Blood Group ……………………………………………
5. Pregnancy (ifapplicable) ……………………………………………………………….

I have examined the above-named student that he/she is physically fit/unfit and mentally*fit/unfit for enrolment as a student teacher.

Date: --------------------------- Signature & Stamp………………………………………

Station …………………………… Designation …………………………..…..…. …………